# MANTIKI KATIKA MIIKO YA MFUMO-MLO YA JAMII YA WANDENDEULE

*Athumani S. Ponera*
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Tanzania*
*atponeraman@gmail.com*

**Ikisiri**

*Makala hii inajadili miiko inayohusiana na mfumo-mlo katika jamii ya Wandendeule. Shabaha kuu ni kubainisha mantiki (kama kipengele kimojawapo cha falsafa) iliyomo ndani ya miiko. Swali kuu lililoongoza uchunguzi na mjadala wa kwenye makala hii ni: miiko kama kipengele cha kiutamaduni ina mantiki gani katika maisha ya wanajamii husika? Makala imejiegemeza katika mkabala wa kitaamuli. Data za makala hii zilipatikana kwa kutumia njia tatu ambazo ni udurusu wa nyaraka, usaili, pamoja na ushuhudiaji. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa miiko yote inayohusu mfumo-mlo inayotumiwa na jamii ya Wandendeule hujikita katika mantiki fulani inayoshikilia seti ya 'kweli' zinazoongoza maisha yao. Hii ni kwa sababu miiko hiyo huakisi uhalisi wa miktadha ya kimazingira (kijiografia), kijamii na kifikra (mawanda ya fikra zao kuhusu ulimwengu).*

## 1.0 Utangulizi

Miiko ni kipengele kimojawapo cha utamaduni wa jamii husika. Makala hii inajadili miiko inayohusiana na mfumo-mlo katika jamii ya Wandendeule (jamii inayopatikana katika mkoa wa Ruvuma, Tanzania). Shabaha kuu ni kubainisha mantiki iliyomo ndani yake. Tunataraji kuwa maudhui ya makala hii yatasaidia jamii kufahamu uzito unaobebwa na miiko. Zaidi, yatapunguza uelewa mwepesi na hasi walionao watu wengi kuhusu dhana ya miiko ya jamii mbalimbali chambilecho Omobola (2013).

Makala imejiegemeza katika utaamuli, yaani imetumia maelezo—na siyo tarakimu—katika kujenga maana ya maudhui yake (Ponera, 2019). Data zilipatikana kwa kutumia njia tatu ambazo ni udurusu wa nyaraka, usaili, pamoja na ushuhudiaji. Hoja kuu inayobainishwa na makala hii ni kuwa, miiko kama kipengele cha kiutamaduni ina mantiki maalumu katika maisha ya Wandendeule. Miiko hugusa mfumo mzima wa maisha ya wanajamii. Aghalabu, mfumo huo mkuu huundwa na mifumo mingine midogomidogo. Kwa kutambua hilo, makala hii imejielekeza kwenye eneo linalohusika na mfumo wa ulaji wa jamii hiyo. Makala imegawika katika sehemu nne ambazo ni: utangulizi, ufafanuzi wa dhana za msingi, uwasilishaji wa data (miiko ya Wandendeule) na mjadala pamoja ya hitimisho.

## 2.0 Ufafanuzi wa Dhana za Msingi

Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa dhana za msingi zinazotumika katika makala hii. Dhana hizo ni falsafa, mantiki, miiko, mfumo-mlo pamoja na Wandendeule.

### 2.1 Falsafa

Falsafa huweza kuelezwa kwa namna tofautitofauti. Katika makala hii tunaitumia dhana hii kwa kuegemea katika maana iliyotolewa na Chuachua (2016) kuwa falsafa ni taaluma ya kutafuta ukweli kuhusu maisha kwa njia ya kutafakari kwa kina. Mhaka (2014) anabainisha kuwa matawi makubwa ya falsafa ni matano. Nayo ni metafizikia (linaloshughulikia mambo yaliyo nje ya upeo wa kujibiwa na sayansi),

semantiki (linaloshughulikia maana ya vipashio mbalimbali vya lugha), aksiolojia (linaloshughulikia thamani kupitia vipengele vya maadili, itikeli na ujumi), epistemolojia (linaloshughulikia chimbuko na maana ya maarifa), na mantiki (linaloshughulikia misingi ya usahihi au utosahihi wa hoja au kauli. Matawi haya yanatokana na mgawanyo ulioasisiwa na kushadidiwa na wataalamu wa Kimagharibi (Wiredu, 2004; Hallen, 2002; Mbiti, 1969).

Falsafa (au seti hiyo ya 'kweli' za maisha) huhusiana na kipengele chochote cha mfumo wa maisha ya wanajamii. Hivyo, huweza kupatikana katika taaluma kama vile sosholojia, dini, fasihi, au utamaduni. Katika makala hii, falsafa inaelezwa kwa kuhusishwa na utamaduni.

## 2.2 Mantiki

Mantiki ni tawi la falsafa linaloshughulikia misingi ya usahihi au utosahihi wa hoja au kauli, kisha kutengeneza mazingira ya kuipa thamani hoja husika kutokana na misingi ya kisayansi. Kwa hiyo, mantiki huweza kuelezwa kuwa ni taaluma inayoshughulikia sayansi ya usahihi wa hoja. Kwa mawanda mapana, mantiki hutazamwa kwa miegamo miwili. Mwegamo wa kwanza huichukulia mantiki kama kiashiria kinachobebwa ndani ya kipashio fulani cha lugha (tungo neno au tungo sentensi). Mwegamo wa pili huichukulia mantiki kama hitimisho la mabunio yanayofikiwa baada ya kukokotolewa kisayansi (kutokana na ithibati za kimuktadha) yanayojengwa kutokana na kufikiri (Jacquette, 2006). Maelezo hayo ya Jacquette yanatubainishia vipengele muhimu vitatu vinavyosaidia kuibuliwa kwa mantiki. Navyo ni maana (semantiki), muktadha maalumu wa matumizi ya kipashio husika, pamoja na ukweli.

Russell (1905) ananukuliwa katika Jacquette (2006) akidai kuwa kwa kawaida, muundo wa nje wa kipashio cha lugha huwa na tabia ya 'kupotosha' maana. Dhana ya kupotosha hapa anaitumia kumaanisha hali ya kuficha mambo yaliyo katika muundo wake wa ndani. Muundo huo wa ndani ndio huwa unabeba vionjo vya kifalsafa. Kuhusu nafasi ya muktadha katika kuibua mantiki, inaelezwa kuwa, aghalabu, jambo lolote hutafsiriwa kulingana na muktadha (wa kiwakati, kimahali, au kitukio) ambamo limetendeka au limetokea. Hii inamaanisha kuwa nje ya muktadha huo huweza kubeba mantiki tofauti. Uhusiano wa kipengele

cha ukweli na mantiki umo katika hoja ya kwamba, kadiri jambo linavyokaribiana na uhalisi/ukubalifu katika akili ya mpokezi ndivyo linavyokuwa na nafasi kubwa ya kujenga mantiki. Makala hii inajadili mantiki iliyomo katika miiko ya mfumo-mlo ya Wandendeule.

## 2.3 Mfumo-mlo

Chakula ni kijenzi muhimu cha afya na uhai wa viumbe hai. Kwa kawaida, chakula huambatana na mambo mengine mengi ambayo humu tunayaita 'mfumo-mlo'. Hivyo, dhana ya mfumo-mlo tunaitumia katika makala hii kumaanisha jumla ya mambo yote yanayozungukia kitendo cha kula. Hii humaanisha kuanzia uzalishaji wa chakula, uandaaji hadi ulaji wenyewe.

Sehemu kubwa ya mambo haya ina uhusiano wa kimfumo. Kwa mfano, jambo linalozungumzia namna fulani ya ulaji, aghalabu huweza pia kutupatia picha kuhusu aina ya chakula hicho. Kwa hiyo, tumeona ni vema tushughulikie dhana ya mfumo-mlo ili kuyabeba kwa pamoja mambo mengine yote yanayoambatana na dhana ya kula. Aidha, dhana za chakula na mfumo-mlo hujengewa maana na thamani kwa kujiegemeza katika utamaduni husika. Miiko ya pote hili ndiyo inayotumika katika makala hii kujadili suala la mantiki.

## 2.4 Miiko

Sehemu hii inafafanua maana, nguzo, mapote na miundo ya miiko.

### 2.4.1 Maana na Chimbuko

Kietimolojia, neno *mwiko* ambalo kisawe chake cha Kiingereza ni *taboo*, linatokana na neno *tabu* la jamii za Wapolynesia zinazopatikana katika Kisiwa cha Tonga kilichopo katika Bahari ya Pasifiki. Maana yake ya msingi ni 'acha kufanya' (Gao, 2013; Kisanji, 2011; Diawuo & Issifu, 2005). Diawuo na Issifu wanaongezea kuwa miiko huwakilisha sheria zisizoandikwa ambazo kazi yake kubwa ni kujenga tabia na mwenendo wa jamii. Kuhusu sababu za makatazo hayo ya kitamaduni, Gao *(khj)* anabainisha kuwa huelekezwa katika vitu, mambo au maeneo yanayoonwa na jamii kuwa ni 'matakatifu' au/na yasiyopaswa kuguswa ovyoovyo. Kwa lugha ya Kindendeule, dhana hii inaitwa *n'hiiro*.

Miiko ya jamii yoyote hutokana na misingi na umri wa utamaduni wa jamii husika (Fershtman, Gneezy & Hoffman, 2009). Omobola (2013) anaongezea kwamba miiko ilianzishwa punde tu wanadamu walipoanza kupambana na mambo mbalimbali yaliyotokea katika mazingira yao. Mambo hayo ni kama vile magonjwa, vifo, fedheha, na misawajiko. Kuwapo kwa mambo hayo kuliamsha urazini wa wanadamu kusaka na kubembeleza jaala njema kwao na kwa vizazi vyao ili kuepusha balaa na majanga. Hivyo:

a) Haiwezi kueleweka nje ya miktadha inayoizunguka jamii husika. Hii ni kutokana na kushikamana kwa miiko na utamaduni;
b) Huwa tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine;
c) Hubadilika kutoka kipindi fulani cha wakati hadi kingine (mabadiliko hayo huweza kutokana na kani za kiteknolojia, kisiasa, au kijamii);
d) Huwa na malengo na dhima maalumu; na
e) Huweza kuwa ya kudumu au ya muda (Freud, 2004 na Holden, 2000)

### 2.4.2 Nguzo za Miiko

Kwa maoni yetu, miiko hushikiliwa na mambo muhimu manne. Mambo hayo ndiyo tunayatambulisha katika makala hii kama ‘nguzo’. Nguzo hizo ni muktadha, katazo, adhabu na kani-uhai.

Nguzo ya muktadha inabeba jumla ya vitu na mazingira yanayotumiwa ndani ya vibebeo (kama vile misemo, methali au vitendawili) vya mwiko husika. Ndani ya vibebeo hivi huwa vinatajwa vitu au mazingira fulani yanayowazunguka na kujulikana bayana na wanajamii husika. Kwa mfano, kuna mwiko usemao: “Ukikalia kinu, utaota majipu makalioni”. Katika mwiko huu, muktadha unahusisha ‘kinu’, ‘majipu’, na ‘makalio’.

Nguzo ya katazo imo katika kitenzi chenye uhasi ‘usikalie’. Nguzo ya adhabu hurejelea jambo au namna yoyote inayoenda kinyume na ridhiko la nafsi ya mtendewa (Peacock na wenzake, 2010). Kwa muktadha wa makala hii, adhabu ni jambo lolote hasi linalotokea kufuatia kukiuka katazo la kitamaduni.

Adhabu hizo, mara nyingi, huwa kubwa, nzito, na zenye kutisha. Kutoka katika mfano wa hapo juu, adhabu ya kukiuka katazo ni kupatwa na majipu katika makalio.

Nguzo ya kani-uhai imo katika hali ya kidhahania. Inarejelea uwezekano wa kutokea kwa adhabu iliyodokezwa katika mwiko husika. Aghalabu, kulingana na simulizi za miiko, sehemu kubwa ya adhabu hiyo hutolewa na wahenga. Wahenga ni watu waliokufa wakiwa watu wazima/wazee na kuacha athari chanya katika jamii husika. Hivyo, huaminiwa kuwa baada ya kufa huwa na uwezo wa kuwasiliana na darala la juu zaidi la kani-uhai (Mungu au Miungu) ili ama kuleta adhabu au neema kwa mtu (Mbiti, 1969; Chuachua, 2016).

### 2.4.3 Miundo ya Miiko

Maelezo kuhusu nguzo za miiko yanatupatia picha ya namna miiko inavyoundwa. Kimuundo, kauli yoyote inayodokeza mwiko huwa na sehemu mbili, katazo na tokeo la ukiukwaji wa katazo. Hata hivyo, mdhihiriko wa sehemu hizi mbili siyo lazima uwe bayana katika miiko yote. Iko baadhi ambayo dhana ya adhabu huwa fiche kutokana na kudondoshwa. Hivyo, kwa umbo la nje, miiko yenye muundo huu huonekana ikiwa na katazo pekee. Adhabu huwa inadondoshwa; na hivyo, hudhihirika kwa umbo la ndani. Kwa mfano, 'Mwiko kumwoa dada yako'.

### 2.4.4 Mapote ya Miiko

Pote ni kundi kubwa la vitu/mambo/fikra (TUKI, 2004). Miiko huweza kugawanywa katika mapote kwa kuzingatia vigezo fotautitofauti. Mgawanyo tunaoutumia katika makala hii umeegemezwa kwa kiasi kikubwa katika fikra zilizotolewa na Allan na Burridge (2006:1) wanaoigawa miiko katika mapote yafuatayo: miiko ya mwili, miiko ya ogani nyeti za mwili na matendo yake, miiko ya magonjwa na kifo, miiko ya majina na miiko ya vyakula. Mgawanyo huu ambao umechukua mwegamo wa kiisimu una matatizo ya kujirudia kwa maudhui. Kwa mfano, miiko ya majina huweza kugusa mwili, ogani nyeti za mwili, na chakula. Kwa maoni yetu, tunamini ni vema kuwa na mgawanyo usiojirudia. Hivyo, tumeupanua mtazamo wao huo na kupata mapote sita

yafuatayo: pote la kiisimu, maadili na itikeli, afya, kazi, uzazi na kifo pamoja na mfumo-mlo. Tutayaeleza kwa kifupi mapote haya kisha kuzamia kwenye pote la mfumo-mlo ambalo ni msingi wa makala hii.

### a) Pote la Kiisimu

Isimu ni taaluma inayochunguza lugha kwa misingi ya kisayansi (Mgullu, 1999). Miiko ya pote hili hujigeza katika matumizi ya lugha katika jamii. Huweka makatazo na adhabu katika namna mbalimbali za kutaja maneno katika miktadha mbalimbali. Kwa kifupi, miiko ya pote hili hufanya kazi ile ile ya tasifida. Mathalani, miiko hii hujielekeza katika utajaji wa sehemu za mwili wa binadamu, hasa sehemu nyeti, utajaji wa michakato ifanywayo sehemu hizo nyeti kama vile kujisaidia au kuzaa, pamoja na utajaji wa mazao yatokanayo na michakato hiyo kama vile kinyesi, mkojo, damu (ya hedhi na ya kawaida) na uteute (Gao, 2013).

### b) Pote la Maadili na Itikeli

Kwa mujibu wa Chuachua (2016), maadili ni seti ya mambo yanayotakiwa kufanywa na mwanajamii ili akubaliwe na mfumo wa maisha ya jamii husika. Itikeli kwa upande wake, ni seti ya maadili iliyokubaliwa itumiwe na kundi fulani la watu (kama vile ualimu, dini, udaktari, utafiti, na jeshi). Miiko ya pote hili hujikita katika kuweka makatazo na adhabu kuhusu masuala kama vile mavazi na uvaaji, uteuzi wa maneno na uongeaji, utoaji na uitaji wa majina kwa watoto, mikao ya watu wa umri na jinsi tofauti katika miktadha mbalimbali, pamoja na aina na namna ya kutoa salamu.

### c) Pote la Afya

Usafi (au uchafu) na magonjwa ni vipengele vinavyohusiana, yaani kuwapo kwa usafi wa miili na mazingira humwepusha mtu au jamii dhidi ya magonjwa. Kinyume chake, uchafu huleta magonjwa. Miiko ya pote hili hujielekeza katika makatazo na adhabu kuhusiana na vipengele vya usafi wa miili, mazingira, pamoja na magonjwa.

**d) Pote la Kazi**

Miiko ya pote hili hujielekeza katika masuala ya kazi. Vipengele vinavyojitokeza ni aina ya kazi (kama vile kilimo, uwindaji, uvuvi, na kazi za nyumbani), mgawanyo wa kazi kulingana na umri na jinsi, namna ya kufanya kazi, pamoja na umuhimu wa kazi).

**e) Pote la Uzazi na Kifo**

Miiko ya pote hili huhusu matukio makubwa mawili ya kuzaliwa na kifo cha mwanajamii. Mhaka (2014) anasisitiza kuwa matukio haya mawili huchukuliwa kwa uzito wa kipekee katika jamii nyingi za Waafrika. Huhusisha matukio kama vile jinsi ya kumhudumia mtoto anapozaliwa, kinga kwa mtoto, na tararibu za mazishi.

**f) Pote la Mfumo-Mlo**

Miiko ya pote hili huhusisha mambo yote muhimu yanayounda mfumo-mlo. Mambo yenyewe ni haya:

i) Uzalishaji wa mazao na mifugo (kuhusu upandaji, uvunaji na uhifadhi);
ii) Aina ya vyakula;
iii) Maandalizi (kuhusu upishi—aina na namna—na maandalizi ya meza);
iv) Ulaji wenyewe; na
v) Kaida za baada ya kula (kuhusu usafi mikono, vyombo, na mahali pa kulia).

## 2.5 Wandendeule

Wandendeule ni mojawapo ya makabila yaliyopo katika nchi ya Tanzania. Kabila hili linapatikana katika mkoa wa Ruvuma, hususani wilaya ya Namtumbo. Wilaya nyingine ambako Wandendeule wanapatikana kwa wingi ni pamoja na Songea (Mjini na Vijijini) na Tunduru. Wilaya ya Namtumbo ina jumla ya wakazi 201,639 (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2013). Etimolojia ya neno ‘ndendeule’ ni tungo-swali ya ‘*ndenda mbhule*’ yenye maana ya ‘nifanye nini?’ au ‘nitafanya nini?’

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mkoa wa Ruvuma (1997), shughuli maarufu ya kiuchumi ya wakazi wa mkoa wa Ruvuma, wakiwamo Wandendeule, ni kilimo. Miongoni mwa mazao maarufu ya biashara wanayolima ni tumbaku, ufuta, maharage na kunde. Kwa upande wa mazao ya chakula, Wandendeule, kama wakazi wengine wa mkoa wa Ruvuma, hulima mahindi, mihogo na mpunga. Ripoti inabainisha zaidi kuwa mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa minne bora katika uzalishaji wa chakula nchini Tanzania (uk. 35).

## 3.0 Uwasilishaji wa Data na Mjadala kuhusu Miiko

Sehemu hii inawasilisha data ya miiko pamoja na mjadala kuhusu mantiki yake.

### 3.1 Miiko ya Mfumo-mlo ya Jamii ya Wandendeule

Tusisitize hapa kuwa kila jamii ina miiko yake. Aidha, miiko ya jamii moja huweza kulandana au kuingiliana kwa namna moja na ya jamii nyingine. Ifuatayo ni miiko ya mfumo-mlo ya Wandendeule iliyokusanywa uwandani:

1. Mwiko kuingiza shambani chombo chenye masizi, mazao 'yatavutwa' na wachawi.
2. Mwiko kula chakula shambani ukiwa umesimama, mazao yatavia.
3. Mwiko kuingia na ndara shambani, maboga yataoza.
4. Mwiko kupekua mahindi yaliyo shambani, mama yako atafanyiwa 'operesheni'.
5. Mwiko kumpa mbegu mtu mkononi, mazao hayatastawi.
6. Mwiko kukalia figa, mama yako atakufa.
7. Mwiko kukalia kinu, utaota majipu makalioni.
8. Mwiko kukalia mchi, utapata ugonjwa wa kizunguzungu.
9. Mwiko kukalia ungo, mama yako atajifungua mapacha.
10. Mwiko kucheza kwenye jiwe la kusagia, ngozi yako itababuka.
11. Mwiko kumpiga mtoto na mwiko, atakuwa kiziwi.
12. Mwiko kutoa au kuomba chumvi usiku, utaita majini.
13. Mwiko kuingiza kisimani sufuria yenye masizi, maji yatakauka.
14. Mwiko kwa mwanamke aliye katika hedhi kuchuma mboga, zitakauka.

15. Mwiko kwa mwanamke aliye katika hedhi kuweka chumvi katika mboga au chakula, mume wake atatenguka[1] miguu.
16. Mwiko kwa mwanamume kukaa kwenye mlango wa jiko, atazuia dada zake kuolewa.
17. Mwiko kukoroga chakula kwa kisu, walaji watahara damu.
18. Mwiko kupakua ugali bila kuuviringa, utachukiwa na watu.
19. Mwiko kupakua ugali kwa kufunika chungu, ndugu zako watapinduka na gari.
20. Mwiko kupitisha chungu nyuma ya wanaume, utajisababishia mikosi.
21. Mwiko kuacha mwiko ukiwa na ukoko, utakuwa huna bahati.
22. Mwiko kulamba kisu, utapata kichomi.
23. Mwiko kwa mtoto kunawa maji kabla ya wakubwa wakati wa chakula, atakuwa hashibi.
24. Mwiko kwa mtoto kuanza kula kabla ya mgeni au mkubwa, hatashiba.
25. Mwiko kwa mtoto kuanza kuchagua nyama, mwili wake utawasha sana.
26. Mwiko kumlisha mtoto mchanga wakati umesimama, utosi wa mtoto utachelewa kuacha kudunda.
27. Mwiko kula ukiwa umesimama, hutanenepa.
28. Mwiko kuongea wakati wa kula, utakula na shetani.
29. Mwiko kula gizani, utakula na wachawi.
30. Mwiko kwa mvulana kulia ugali kwenye chungu, hatapata mwanamke wa kumwoa.
31. Mwiko kwa mwanamke mjamzito kula mayai, atazaa mtoto mwenye kipara.
32. Mwiko kwa mwanamke kula nyama ya mnyama mwenye mimba, atakuwa anajifungua kwa tabu.
33. Mwiko kwa mwanamume kukomba mwiko, ataota matiti.
34. Mwiko kuonja muhindi ulioanza kuiva upande mmoja, utaugua ugonjwa wa meno.

---

[1] Kwa mujibu wa TUKI (2004), *kutengua* ni kuondoa uhalali, kutenganisha vitu—aghalabu, kwa nguvu—kiasi cha kusababisha madhara. Maana hii huendana na ya ‘kuteguka’. Katika makala hii kutenguka kumetumiwa kijazanda kumaanisha hali kama vile ya kuishiwa nguvu, kuharibika kwa kitu kilicho katika ruwaza fulani.

## 3.2 Uchanganuzi wa Data

Data hii ya miiko thelathini na minne (34) inagusa vipengele muhimu vya mfumo-mlo. Kuhusu muundo, miiko yote imebeba sehemu mbili muhimu za katazo na adhabu. Kuhusu walengwa, data ya miiko inaonesha kugawika katika makundi mawili: Mosi, kundi linalobainisha walengwa waziwazi. Uwazi unaorejelewa hapa unaweza kutokana na kutajwa moja kwa moja au kwa kutumia ithibati ya baadhi ya vipashio vilivyomo katika mwiko husika. Kulingana na data yetu, kundi linalobainisha walengwa kwa uwazi linagusa makundi yafuatayo: watoto, watu wazima, wanawake, na wanaume. Pili, kuna kundi lenye walengwa fiche. Miiko ya kundi hili inaweza kumgusa yeyote. Hii ni kwa sababu huwa haijielekezi moja kwa moja kwa ama mtoto, mtu mzima, mwanamke au mwanamume.

Kuhusu miktadha ya kuundia miiko, data iliyokusanywa inaonesha kuwa miiko ya Wandendeule imeundwa kwa kutumia dhana zinazohusiana na jamii hiyo. Dhana hizo (mifano yake imefungiwa katika mabano) ni kama vile viambata vya teknolojia ya kupata unga wa kusongea ugali (kupitia kusaga kwenye mawe au kutwanga—jiwe, kinu, na mchi), shughuli za kilimo (shamba, mazao), vyakula vyao maarufu (ugali), pamoja na desturi (kuoa, kuolewa na kuzaa). Kwa upande wa aina ya adhabu zinazotokana na kukiuka makatazo, data inaonesha kuwa: mosi, kila katazo limewekewa adhabu yake ambayo inashabihiana nalo kimazingira. Kwa mfano, makatazo ya miiko namba 4 na 34 yametumia dhana za ‘kuonja muhindi ulioanza kuiva upande mmoja’, na ‘kupekua mahindi yaliyo shambani’.

Kwa upande wa adhabu zake, zimetumiwa dhana za ‘mama wa mtenda kufanyiwa ‘operesheni’ na ‘kuugua ugonjwa wa meno’. Hapa kuna kushabihiana kwa kiasi kikubwa kati ya dhana iliyopo katika katazo na ile ya adhabu. Kitendo cha ‘kupekua mahindi yaliyo shambani’ (kupasua kidogo maganda ya mhindi ulio katika hali ya mashaka ya kukomaa ili kujiridhisha kabla ya kuuvuna kwa ajili ya matumizi) kinashabihiana na kitendo cha upasuaji anaofanyiwa mgonjwa hospitali kwa ajili ya tiba. Pia, uonjaji (utafunaji) wa mahindi yakiwa bado hayajaiva sawasawa unahusishwa na ugonjwa wa meno (ambayo ndiyo zana muhimu ya kutafunia).

Adhabu hizo, kadiri ya data ya hapo juu, zinaonekana kuwa katika darajia tofauti tano zifuatazo:

a) Kuharibika kwa mazao;
b) Kupatwa na kadhia za kidhahania kama vile kuadhibiwa na majini, mashetani na wanga au 'kulazimishwa' kushirikiana nao katika shughuli kama vile kula;
c) Kupatwa na madhara ya kijamii kama vile kutopata mke, mume au mtoto; pamoja na kuwa na mkosi (kama vile kuchukiwa na watu, au kukosa bahati katika maisha kwa ujumla);
d) Kupatwa na maradhi ya kutisha kama vile ngozi kubabuka, kupata majipu makalioni, na madhara ya kimaumbile kama vile upara au ulemavu; na
e) Kifo.

Adhabu hizi zimepangwa kuanzia nyepesi, za kati, nzito, na nzito zaidi. Utaratibu wa kuambatisha aina fulani ya adhabu katika katazo unatudokezea kiwango cha unyeti wa mantiki iliyomo katika mwiko husika.

Zaidi ya hayo, data hiyo inatuonesha kuwa miiko takribani yote imepambwa na lugha ya kiujumi inayohusianisha mambo au dhana. Mifano mizuri ni uhusiano wa jozi zifuatazo: masizi a uchawi au mkosi, kulamba kisu na kupata kichomi, kukomba mwiko na kuota matiti, na kugubika (kufunika) chungu na kupinduka kwa gari. Namna hii ya uhusianishaji huwasaidia sana wanajamii katika kuielewa na kuikumbuka miiko husika.

## 3.3 Mjadala Kuhusu Mantiki Iliyomo katika Miiko Husika

Mjadala wa mantiki iliyomo katika miiko ya Wandendeule unajigeza katika fikra mbili za Jacquette (2006) kama zilivyodondolewa hapo juu (kutumia viashiria vilivyomo katika miiko husika pamoja na mabunio yanayotokana na fikra za wahusika wa miiko hiyo ili kuibua mantiki ya matini husika). Mjadala umeigawa miiko hiyo katika makundi makubwa manne yafuatayo: Miiko inayohusu maandalizi ya mazao shambani, inayohusu ukusanyaji wa vifaa vya mapishi na vyakula, inayohusu taratibu za mapishi, pamoja na ile inayohusu taratibu za ulaji. Baadhi ya

miiko mantiki yake inalandana; hivyo, ili kuepuka uradidi, imejadiliwa kwa pamoja.

### A. Miiko Inayohusu Maandalizi ya Mazao yakiwa Shambani

Mantiki ya miiko ya kundi hili inajielekeza katika kuhakikisha kuwa jamii inakuwa na chakula cha kutosha kwa kipindi chote cha mwaka. Ili kuhakikisha jambo hili linatokea, jamii hutumia miiko kudhibiti shughuli za ulimaji, upandaji, na ulinzi wa mazao. Miiko yenyewe ni hii:

#### 1. Mwiko kuingiza shambani chombo chenye masizi, mazao 'yatavutwa' na wachawi

Masizi, katika mwiko huu, yanatumika kama jazanda ya mkosi. Hii ndiyo sababu adhabu yake inanasibishwa na shughuli za wachawi. Masizi hupatikana katika chungu au sufuria inayotumika kwa kupikia, hususani mapishi ya kutumia jiko la kuni au mkaa. Sura ya ndani ya mwiko huu inatuibulia dhana ya umakini katika uteuzi wa vifaa vya kufanyia kazi. Hakuna shughuli yoyote ya shambani ambayo inaweza kuruhusu matumizi ya sufuria au chungu. Kinyume chake, ubebaji wa sufuria au chungu wakati wa shughuli kama vile kuchuma mboga au kuvuna mahindi huchukuliwa kama uvivu. Hivyo, hili ni katazo la uvivu; kwamba, wahusika hutakiwa kuchukua vifaa vikubwa kama vile makapu, mifuko au magunia kwa ajili ya kazi husika.

#### 2. Mwiko kula chakula shambani ukiwa umesimama, mazao yatavia

Hili ni kemeo jingine kuhusu uvivu. Chimbuko la mwiko huu ni wakati wa kulima. Wandendeule, kama zilivyo jamii nyingine za wakulima, hutumia takribani saa kumi kwa siku wakiwa mashambani. Hivyo, chakula huliwa wakiwa hukohuko. Wavivu huwa na tabia ya kula polepole, tena wakiwa wamesimama. Zaidi ya uvivu, mwiko huu unajenga tabia ya heshima. Kwa Wandendeule, ulaji wa wima (iwe shambani au nyumbani) ni kiashiria cha dharau kwa mpishi na jamii kwa ujumla. Fikra hii pia ipo katika jamii nyingine za Watanzania. Mathalani, Kisanji (2011) anabainisha kuwapo kwa wazo kama hili katika jamii ya Wabungu (wa mkoani Mbeya). Anasema kuwa Wabungu hutakiwa kula wakiwa wamekaa ili kuheshimu chakula.

### 3. Mwiko kuingia na ndara shambani, maboga yataoza

Umbo la ndani la mwiko huu limebeba angalizo kuhusu usafi wa vyakula vilivyo shambani pamoja na umakini ili kutoharibu mazao yanayotambaa au mazao ya chini kama vile kunde, mbogamboga na karanga. Wandendeule wana kawaida ya kupanda mazao mchangayiko katika shamba moja. Kwa mfano, shamba moja huweza kupandwa mahindi, miboga na mikunde; au huweza kuchanganywa mpunga na miboga. Adhabu ya 'kuoza kwa maboga' imetumika hapa kutokana na ukweli kuwa miboga hupandwa sana na wakazi wa Mkoa wa Ruvuma. Majani yake ni mboga maarufu (*pitiku*) na matunda yake (maboga) ni chakula. Hivyo, kutokana na ukweli kuwa vazi la ndara hurusha mchanga, watu—hasa watoto—huzuiwa kwenda nazo mahali palipopandwa mazao ya jinsi hiyo ili kutoyachafua kwa mchanga, hivyo kuharibu mboga (*pitiku*).

### 4. Mwiko kupekua mahindi yaliyo shambani, mama yako atafanyiwa 'operesheni'

Mahindi ni miongoni mwa mazao maarufu ya chakula yanayolimwa na Wandendeule. Watoto huwa na kawaida ya kupekua mahindi yanapokuwa katika hatua ya kuelekea kukomaa. Kitendo hiki huyaacha mahindi yasiyokomaa yakiwa wazi, hatimaye kuoza au kuliwa na wadudu, wanyama au ndege waharibifu. Hali hii ndiyo iliyosababisha kuanzishwa kwa mwiko huu. Shabaha kuu ni kuyalinda mazao hayo ili yakomae ndipo yavunwe kwa ajili ya kuliwa (ama kwa kuchomwa au kusagwa unga).

### 5. Mwiko kumpa mbegu mtu mkononi, mazao hayatastawi

Chimbuko la mwiko huu ni zoezi la kuotesha mbegu shambani. Huweza kutokea wakati fulani mtu akaishiwa mbegu na kulazimika kuomba kwa mwenzake. Mwiko umejiegemeza kwenye imani ya Wandendeule kuhusu 'mkono' (bahati) katika kilimo. Kwa mujibu wa Bibi Chiku Ngonyani[2], Wandendeule huamini kuwa kila mtu ana 'mkono' wake katika mazao mbalimbali; yaani, fulani anapootesha zao fulani hupatikana mavuno

[2] Mahojiano ya simu yaliyofanyika kati ya mwandishi na Bibi Chiku Ngonyani (miaka 52) yaliyofanyika Aprili 18, 2017. Bibi Chiku ni mkazi wa kata ya Rwinga, Namtumbo, Ruvuma.

mengi. Mathalani, wapo wanaoaminika kuwa na ‘mkono’ wa maboga, ‘mkono’ wa viazi, ‘mkono’ wa mahindi, au ‘mkono’ wa mpunga. Hivyo, kitendo cha kumpa mtu mbegu mkononi ili azioteshe huchukuliwa kuwa ni sawa na ‘kuchanganya mikono’. ‘Uchanganyaji huo wa mikono’ huzuiwa kwa sababu mbili: Mosi, kuondoa hali ya kutojulikana kwa uwezo au bahati ya mtu katika kuotesha mazao. Pili, na kubwa zaidi, ni kuzuia mkanganyo wa bahati za watu zaidi ya mmoja katika zao moja. Njia ya kupeana mbegu inayoafikiwa na jamii hii ni kumwekea mwingine chini ili azichote au aziokote. Kwa kufanya hivi, jamii huamini kuwa ardhi huwa imezitakasa mbegu kabla hazijaingia katika mikono ya mpandaji mpya (hivyo, ‘mkono’ wake unabakia vilevile bila kuchafuliwa).

Kwa umbo la ndani, mwiko huu unatumulikia dhana ya umuhimu wa maandalizi ya mbegu katika mchakato wa kilimo. Kinachosisitizwa hapa ni umakini katika maandalizi ya mbegu za kutosha. Kila mmoja anapaswa kuweka mbegu za kutosha katika chombo chake kabla ya kuanza zoezi la kuotesha. Kufanya hivi, kwa upande mwingine, huimarisha maarifa na stadi za kufanya makadirio ya shughuli za kilimo.

### B. Miiko Inayohusu Vifaa kwa ajili ya Mapishi pamoja na Ukusanyaji wa Vyakula

Kundi hili linajumuisha miiko inayohusisha maandalizi ya mboga, unga, chumvi na maji. Pia, huhusisha vifaa vingine kama vile vinu, michi, miiko ya kupikia, na mawe ya kusagia. Miiko yenyewe ni hii:

6. Mwiko kukalia figa, mama yako atakufa.
7. Mwiko kukalia kinu, utaota majipu matakoni.
8. Mwiko kukalia mchi, utapata ugonjwa wa kizunguzungu.
9. Mwiko kukalia ungo, mama yako atajifungua mapacha.
10. Mwiko kucheza kwenye jiwe la kusagia, ngozi yako itababuka.
11. Mwiko kumpiga mtoto na mwiko, atakuwa kiziwi.

Mantiki ya miiko yote hii sita (mwiko namba 6 hadi 11) ni kujenga tabia ya usafi katika mchakato wa kupatikana kwa chakula. Zana zote zinazotajwa katika makatazo hayo (figa, kinu, mchi, ungo, mwiko, na jiwe la kusagia) hutumika katika mchakato wa kuandaa chakula. Kwa

teknolojia iliyokuwepo hapo zamani wakati miiko inazaliwa, kinu, mchi, ungo na jiwe gumu la kusagia vilikuwa vya lazima katika kila familia ili kuwezesha kupatikana kwa unga au mchele. Katika mazingira ya vijijini, teknolojia hii ya kuitumia mashine rahisi inaendelea kutumika hadi hivi leo ama kutokana na kukosa mashine tata (za kisasa) za kusagia au kutokana na imani kuhusu unga utokanao na kutwangwa katika kinu au kusagwa kwenye jiwe. Uchunguzi umebaini kuwapo kwa baadhi ya wakazi ambao hawali chakula kilichosagwa katika mashine tata kwa vile kina vipande vya chuma (vinavyotokana na kwisha kwa meno yanayopondaponda nafaka au machekeche yanayochuja unga katika mashine hizo).

Unyeti wa suala la usafi wa chakula unadhihirika kupitia adhabu zinazowekwa kwenye miiko husika. Adhabu za kuvunjwa kwa makatazo hayo ni nzito na huwaogofya wanajamii, hususani watoto, ili wasithubutu kuvunja miiko husika. Kifo, kupatwa na maradhi kama vile kubabuka ngozi na majipu (tena katika makalio), pamoja na kujifungua watoto mapacha (uzazi wa jinsi hii unaogopwa na watu wengi kutokana na ama kadhia za kujifungua—kutokana na teknolojia ya wakati huo—au uzito wa malezi ya watoto) ni adhabu zinazolenga kuwatisha na kutoa uzito kwenye mantiki ya makatazo husika. Mbali na mantiki ya kusisitiza usafi, hapa tunapata pia suala la usalama kwa wanajamii. Mafiga huwa na joto kali baada ya kutumika; hivyo, kama mtu atakuwa na tabia ya kuyakalia ovyo, ni rahisi kuungua makalioni ikiwa atakalia ambalo halijapoa. Kwa upande mwingine, uduara wa maumbile ya vinu na michi huweza kusababisha hatari kwa watu wanaochezea au kukalia (kutokana na kuwapo kwa uwezekano wa kuviringika na kuwaangusha). Dhana hii ya kuviringika, kwa maoni ya mwandishi wa makala hii, inaumana vyema na dhana ya ‘ugonjwa wa kizunguzungu’ inayojitokeza katika mwiko namba 8. Mwangwi wa mantiki ya usalama unajitokeza pia katika mwiko namba 11. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mwiko hutengenezwa kwa miti migumu na imara. Hivyo, itumikapo kumpigia mtu mwingine ni rahisi kumuumiza au hata kumuua. Kwa hiyo, dhana ya ‘u-kiziwi’ katika adhabu ya kuvunjwa kwa mwiko husika imetumika kama tasifida ya ajali ya kuumizwa kwa mtu au kuuwawa.

**12. Mwiko kutoa au kuomba chumvi usiku, utaita majini**

Chumvi ni kiungo kikuu na cha lazima katika mapishi. Ukuu na ulazima huo ndio uliozua dhana za ‘heshima ya jiko’ au ‘dawa ya jiko’ ambazo zinaipaza hadhi yake. Kutokana na hadhi hiyo, ni wazi kuwa kila apikaye lazima aweke makini kuhusu kuwapo kwake na kiwango cha matumizi katika chakula husika. Katika mwiko huu, kwa ndani tunauona msisitizo wa mwanamke kuwa makini katika kufanya maandalizi ya chakula, hasa cha usiku. Imedokezwa mwanzoni kwa makala hii kuhusu umashuhuri wa shughuli za kilimo kwa Wandendeule. Sehemu kubwa ya wakulima hudamka alfajiri na kwenda kulima. Kipindi hiki huenda hadi saa za mchana ambapo hupumzika kutokana na jua kuwa kali, kisha, saa za alasiri hurejea tena shambani kulima hadi jua linapozama; hatimaye, hurudi nyumbani. Ni katika kipindi hiki ndipo mwanamke asiye makini huweza kujikuta anarudi nyumbani na kuanza kukusanya vitu muhimu kama vile chumvi na mboga ili kuwezesha kupatikana kwa chajio cha familia yake. Kwa hiyo, kwa mawanda mapana, dhana ya chumvi imetumika kama jazanda ya jiko kwa ujumla. Pia, ‘majini’ yametumika kijazanda kumaanisha matatizo. Chukulizi ya jumla hunasibisha majini na giza/usiku. Kitendo cha mwanamke kujikuta anahaha usiku kusaka vitu vinavyohusiana na mapishi (kama vile kuomba chumvi) ambavyo katika hali ya kawaida alitakiwa awe amekwishaviandaa mapema humwondolea heshima mbele ya mume wake na jamii kwa ujumla (kuita majini).

**13. Mwiko kuingiza kisimani sufuria yenye masizi, maji yatakauka**

Umbo la ndani la mwiko huu limebeba suala la kusisitiza usafi kwa wanajamii. Tangu kale jamii ya Wandendeule ilitegemea visima, mito pamoja na mifereji kama vyanzo vya kuwapatia maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ikiwamo kunywa. Masizi, kama ilivyoelezwa hapo juu, ni jazanda ya mambo hasi kama vile mkosi na uchafu. Maji ni uhai, hivyo mwiko huu unazuia kitendo cha kuingiza mkosi au uchafu katika kitovu cha uhai. Ndiyo maana adhabu yake imeelekezwa katika kuzimwa kwa uhai (maji kukauka).

**14. Mwiko kwa mwanamke aliye katika hedhi kuchuma mboga, zitakauka**

Gao *(khj)* anabainisha kuwa miiko huelekezwa katika vitu, mambo au maeneo yanayoonwa na jamii kuwa ni matakatifu au maalumu, hivyo hayapaswi kuguswa ovyoovyo. Hedhi ni miongoni mwayo; ndiyo maana kuna miiko mingi inayohusiana nayo (katika pote la mfumo-mlo na mapote mengineyo).

Kokote unakojitokeza mwiko unaogusia hedhi, umbo lake la ndani hubeba heshima, thamani maalumu, huruma, na usafi. Kuhusu heshima, hedhi huchukuliwa na jamii kama tukio maalumu linalomtokea mwanamke kila mwezi. Dhana ya huruma hutokana na ukweli kuwa hedhi, kwa baadhi ya wanawake, huambatana na kadhia ya maumivu. Hivyo, baadhi ya miiko ilianzishwa ili kuwapunguzia majukumu, hatimaye wapate muda wa kupumzika. Suala la usafi linarejelea njia na nyenzo zilizokuwa zinatumika katika kujihifadhi wakati wa tukio la hedhi. Maendeleo ya kiteknolojia hivi sasa yanawawezesha wasichana na wanawake kuwa na vifaa vinavyowawezesha kujihifadhi kwa namna nyepesi inayohakikisha staha, faragha na usafi.

Kwa hiyo, umbo la ndani la mwiko huu linadokeza usafi na huruma. Utafutaji na uchumaji wa mboga ni kazi ngumu. Mwanamke hutakiwa wakati mwingine kutembea umbali mrefu kuelekea liliko shamba. Aidha, kutokana na teknolojia duni iliyokuwapo, wanawake, hasa wasichana wadogo, waliokuwa wanaingia katika hali hiyo walihofiwa kutokuwa katika hali nzuri ya kiusafi.

**C. Miiko inayohusu Mapishi**

Kundi hili limejadili miiko inayohusisha eneo la kupikia pamoja na kunga za kitendo chenyewe cha kupika. Miiko yake ni hii:

### 15. Mwiko kwa mwanamke aliye katika hedhi kuweka chumvi katika mboga au chakula, mume wake atatenguka miguu

Akifafanua maana ya mwiko huu pamoja na uhusiano kati ya katazo na adhabu yake, Bibi Mbawala[3] anasema:

> Mwiko huu ulikuwa unawasisitiza wanawake kuwa wasafi wakati wakiwa katika siku zao. Wanazuiwa kushika chumvi na vyakula vingine ili wasisambaze uchafu kwa watu wengine. Hivyo, watoto ndiyo hutumwa kufanya hivyo... ikitokea bahati mbaya mwanamume akagusa au kula ule uchafu anatenguka miguu.

Kisayansi, uchafu unaotoka wakati mwanamke akiwa katika siku zake huwa na madhara kiafya ikiwa utaliwa. Kwa maoni ya mwandishi wa makala hii, dhana ya ‘kutenguka miguu’ hapa imetumika kama tasifida ya kupoteza nguvu za kiume. Hivyo, kwa kuchelea jambo hili kutokea kwa waume zao, wanawake huwa makini sana kuuzingatia mwiko huu. Hivyo, mantiki iliyomo katika mwiko huu inalandana na ile iliyoelezwa katika mwiko namba 14 hapo juu.

### 16. Mwiko kwa mwanamume kukaa kwenye mlango wa jiko, atazuia dada zake kuolewa

Mantiki ya mwiko huu ni kujenga mgawanyo wa majukumu pamoja na kutengeneza mazingira mazuri na huru ya kutekeleza majukumu. Jikoni ni eneo lilalotumika kwa ajili ya kuandalia vyakula. Kwa kawaida, wahusika wa mapishi (wanawake na wasichana) huwa huru katika mavazi, mazungumzo na mikao wawapo huko. Kwa hiyo, kuwapo kwa mwanamume au mvulana katika eneo hilo huweza kukwaza uhuru wao katika vipengele hivyo (mavazi, mazungumzo na mikao).

Kwa upande mwingine, katazo la mwiko huu limebeba dhana ya usalama wa wapishi. Nje ya pote hili la mfumo-mlo, upo mwiko mwingine wa jumla unaolandana na huu, unasema: ‘Mwiko kukaa mlangoni, familia itapata mikosi’. Mantiki ya jumla hapa ni kuimarisha ulinzi na usalama

---

[3] Bibi Mbawala (miaka 71) ni mkazi wa Lumecha, Kata ya Msindo, katika Wilaya ya Namtumbo. Mahojiano na mwandishi yalifanyika Machi 25, 2017.

dhidi ya ajali yoyote inayoweza kutokea. Mathalani, nyumba nyingi zilikuwa zimeezekwa kwa nyasi, hivyo kuwapo kwa uwezekano wa kutokea kwa ajali ya moto muda wowote. Pia, wilaya ya Namtumbo ipo karibu na Mbuga ya Wanyama ya Selous. Matukio ya uvamizi wa wanyama katika makazi ya watu yalikuwa yanatokea mara kwa mara wakati huo. Hivyo, muda wote milango ilitakiwa iwe wazi na huru ili kuruhusu watu kujiokoa kwa urahisi pale inapohitajika.

17. **Mwiko kukoroga chakula kwa kisu, walaji watahara damu**

18. **Mwiko kupakua ugali bila kuuviringa, utachukiwa na watu**

19. **Mwiko kupakua ugali kwa kufunika chungu, ndugu zako watapinduka na gari**

20. **Mwiko kupitisha chungu nyuma ya wanaume, utajisababishia mikosi**
21. **Mwiko kuacha mwiko ukiwa na ukoko, utakuwa huna bahati**

Miiko hii mitano (namba 17 hadi 21) inamlenga mwanamke. Maumbo yake ya ndani yamebeba ujumi wa mapishi ya Wandendeule, usafi wa chakula, pamoja na usalama wa wapishi na walaji. Ujumi wa mapishi umebebwa katika miiko namba 18, 19 na 21. Mwanamke wa Kindendeule hutakiwa kuzingatia taratibu pamoja na ujumi wa mapishi ya jamii hiyo ikiwa ni pamoja na usafi wa vyombo kabla na baada ya mapishi na kula. Kipengele kingine cha ujumi wa mapishi ya Wandendeule ni mwonekano wa ugali (ugali unatajwa moja kwa moja hapa kwa sababu hiki ndicho chakula chao kikuu) ukiwa katika sahani au sinia kama inavyosawiriwa katika mwiko namba 18. Ugali ukiwa umeviringwa vizuri humaanisha heshima; kinyume chake, mwanamke (ambaye ndiye mpishi) hupoteza heshima yake mbele ya mume au/na jamii. Miiko namba 18 na 19 inaendana kimantiki, kwani ikiwa ugali utaipuliwa kwa namna ya kugubika sufuria au chungu, utakosa umbo zuri na la kiheshima uwapo ndani ya sahani au sinia. Hata hivyo, njia hii ya kuuipua ugali huweza kusababisha hatari kubwa ya kumwagika kwa ugali kutokana na haraka

ya mpishi kuogopa kuunguzwa na sufuria iliyotoka motoni. Adhabu iliyowekwa (ya ndugu wa mvunja mwiko huu kupinduka na gari) inaakisi ukubwa wa hatari hiyo.

Mwiko namba 20 unaonya kuhusu hatari ya kuwamwagia na kuwaunguza watu ikiwa itatokea bahati mbaya yoyote wakati chungu chenye chakula kinapitishwa mgongoni. Hii ni kwa sababu anayepitishiwa hataweza kukwepa au kujiokoa kwa urahisi kwa kuwa hana uwezo wa kuona vitu vilivyo nyuma yake.

### 22. Mwiko kulamba kisu, utapata kichomi

Mantiki ya mwiko huu inaendana na ya mwiko namba 17 hapo juu. Kisu ni kifaa chenye makali kinachotumika kukatia vitu mbalimbali, vikiwamo vyakula. Mathalani, watoto wa jamii ya Wandendeule hupenda kutumia kisu kumenyea na kukatia maembe; na, huweza kula vipande hivyo vya maembe vikiwa kwenye kisu. Tabia hii huweza kusababisha wajikate. Aidha, huweza kuvichafua visu kwa mate yao. Hivyo, mantiki ya mwiko huu na wa hapo juu imo katika kuhakikisha usafi na usalama wa watumiaji wa kisu.

## D. Miiko inayohusu Taratibu za Ulaji

Miiko ya kundi hili huhusu vipengele vifuatavyo: aina ya vyakula, nani ale nini, muda wa kula, mikao ya kula, pamoja na namna ya kula. Idadi ya miiko ya kundi hili ni kubwa kuliko ya makundi mengine. Hii, kwa maoni ya mwandishi, ni kwa sababu ya upekee wa dhana ya kula kwa jamii nyingi za Kitanzania, wakiwamo Wandendeule.

Kitendo cha kula huhusishwa na vipengele muhimu vinavyomzunguka mwanadamu kama vile afya, utamaduni, pamoja na tabia yake (ukarimu au uchoyo). Afya ya mtu hutokana na anachokula na anavyokula. Pia, tofauti ya aina ya vyakula na namna ya kula ni msingi mmojawapo unaoitofautisha jamii moja na nyingine. Zaidi, namna binafsi ya ulaji wa mtu ni kipengele kimojawapo muhimu cha kuitambulisha tabia yake. Kutokana na data iliyokusanywa, ifuatayo ni miiko ya kundi hili:

**23. Mwiko kwa mtoto kunawa maji kabla ya wakubwa wakati wa chakula, atakuwa hashibi**

Mantiki iliyofichwa katika mwiko huu ni umuhimu wa usafi. Mara nyingi watoto huwa na michezo mingi inayoweza kuifanya mikono yake iwe michafu sana kuliko watu wazima. Mwiko huu unarejelea wakati ambao watu walikuwa wananawa maji yaliyotiwa ndani ya chombo kimoja. Hivyo, wakubwa walitakiwa watangulie kunawa kwa kuwa walikuwa wana unafuu wa uchafu mikononi (kuliko watoto), ndipo watoto wafuatie. Zaidi ya hayo, ikiwa mtoto alitangulia kushiba, alitakiwa asubiri kwa kuendelea kula taratibu hadi mkubwa ashibe. Desturi hii ya Wandendeule inasaidia kudumisha heshima kati ya mkubwa na mdogo. Pia, humwezesha mtoto kuondoa vyombo mara tu baada ya mkubwa kumaliza kula.

**24. Mwiko kwa mtoto kuanza kula kabla ya mgeni au mkubwa, hautashiba**

Mantiki iliyobebwa katika mwiko huu inalandana na iliyoelezwa katika mwiko namba 23 hapo juu. Hii ndiyo sababu hata adhabu ya uvunjifu wa mwiko huo ni moja (kutoshiba). Adhabu hii, kwa mujibu wa darajia za adhabu za miiko ya Wandendeule, iko katika darajia ya chini.

**25. Mwiko kwa mtoto kuanza kuchagua nyama, mwili wake utawasha sana**

Suala la heshima kwa wakubwa linajitokeza tena katika mwiko huu. Mtu mzima alipaswa kuwa wa kwanza kuchagua nyama aipendayo, kisha watoto wanafuatia kwa kuchukua kile ambacho kimebaki. Tofauti kati ya mwiko huu na miiko namba 23 na 24 inaonekana katika ngazi ya adhabu. Adhabu ya mwiko huu (‘mwili kuwasha sana’) inaonekana kuwa kubwa ilikinganishwa na ya miiko hiyo mingine miwili (‘kutoshiba’). Hii inamaanisha kuwa katazo la mwiko huu ni kubwa kuliko hayo mengine.

**26. Mwiko kumlisha mtoto mchanga wakati umesimama, utosi wa mtoto utachelewa kuacha kudunda**

**27. Mwiko kula ukiwa umesimama, hautanenepa**

Makatazo ya miiko hii miwili (namba 26 na 27) yanalandana sana. Imefafanuliwa katika mwiko namba 2 kuwa mantiki ya mwiko huu ni kusisitiza adabu ya kula. Zaidi ya ufafanuzi huo, mantiki ya mwiko huu

inaoana na misingi ya kidini inayoeleza kuwa mpangilio wa chakula tumboni huwa mzuri zaidi ikiwa mlaji atakuwa amekaa kuliko kusimama (An-Nawawy, 2008: 518-519). Idadi kubwa ya Wandendeule ni Waislamu. Hivyo, kuwapo kwa miiko hii kunaweza kuhusishwa na maarifa yanayotokana na imani hiyo.

**28. Mwiko kuongea wakati wa kula, utakula na shetani**

Mantiki ya mwiko huu ni kudumisha usafi na afya ya walaji. Kuongea wakati wa kula huweza kusababisha kupaliwa (baada ya vipande vya chakula kuingia katika njia ya hewa). Pia, huweza kusababisha mzungumzaji kutemea mate katika chakula au kuwatemea wenzake. Hivyo, kupitia mwiko huu wanajamii, hasa watoto, hujengewa adabu ya kula.

**29. Mwiko kula gizani, utakula na wachawi**

Mambo yanayobebwa katika umbo la ndani la mwiko huu ni ukarimu, adabu za kula, pamoja na usalama wakati wa kula. Wandendeule na Waafrika kwa ujumla wana kawaida ya kushirikiana katika mambo mengi, likiwamo suala la chakula na kula. Ulaji wa chakula ni jambo linalopaswa kufanyika hadharani (mara nyingi ni mbele ya nyumba) ili kutoa fursa kwa wapita njia au majirani kula. Katika kuhakikisha kuwa wanawajengea watoto mazoea ya kuwa wakarimu na kuwaepusha na choyo, mwiko huu ulianzishwa. Zaidi, kula katika mahali panapoonekana kuliwawezesha wazazi au walezi kuendelea kuisoma mienendo ya watoto katika ulaji, hivyo kuweza kuwarekebisha pale ilipobidi. Kuhusu suala la usalama wakati wa kula, mwiko huu unalenga kuwalinda walaji, hasa watoto, wasije kula chakula na vitu hatarishi vinavyoweza kudhuru afya na uhai wao kama vile miiba (ya samaki), mifupa ya nyama au wadudu wanaoweza kuwamo katika chakula. Ili kuonesha msisitizo, imewekwa adhabu inayohusisha suala la uchawi au wachawi. Dhana ya uchawi ni miongoni mwa mambo yanayowaogofya watoto; hivyo, kuwafanya wajenge tabia ya kula hadharani na penye mwanga.

**30. Mwiko kwa mvulana kula ugali kwenye chungu, hatapata mwanamke wa kumwoa**

Mwiko huu unaturudisha katika teknolojia ya kutumia vyungu kwa ajili ya kupikia. Mantiki inayojitokeza hapa ni usalama wa chombo. Kwa kiasi kikubwa, suala la mapishi hufanywa na wasichana na wanawake; hivyo, hawa ndio walionekana kuwa makini na utunzaji wa vyungu na mitungi iliyokuwa inatumika. Kutokana na wavulana kutokuwa karibu na matumizi ya vyombo hivi pamoja na kuwa na silika ya papara waliyonayo, walionekana kuwa waharibifu mara kwa mara walipokuwa wanavitumia. Hivyo, mwiko huu ni kinga maalumu kwa uharibifu wa jinsi hiyo. Aina ya adhabu iliyowekwa kwa wavunjaji wa mwiko huu (‘kukosa mwanamke wa kumwoa’) inaendana na hulka ya wavulana hao (ya kupenda wasichana), pamoja na fikra za jamii nzima kuhusu maana na thamani ya ndoa. Hivyo, kurahisisha utekelezaji wa mwiko husika.

**31. Mwiko kwa mwanamke mjamzito kula mayai, atazaa mtoto mwenye kipara**

**32. Mwiko kwa mwanamke kula nyama ya mnyama mwenye mimba, atakuwa anajifungua kwa tabu**

Miiko hii miwili (namba 31 na 32) inahusu suala adhimu la uzazi. Kila mwanajamii hupenda mwanamke mjamzito ajifungue kwa urahisi na ajifungue mtoto asiye na kasoro. Mwiko namba 31 unaturejesha katika zama za teknolojia duni ya ukunga, ambapo ujuzi wa upasuaji katika jamii ya Wandendeule, na jamii nyingine nyingi nchini Tanzania, haukuwepo. Hivyo, wanawake wengi waliokuwa wanakula vyakula vyenye protini, kama vile mayai na nyama, walikuwa na uwezekano mkubwa wa kupoteza maisha wakati wa kujifungua pale ilipotokea mtoto kuwa na umbo kubwa kuliko njia ya mama. Hivyo, mantiki ya mwiko huu imo katika ulinzi na usalama wa afya ya mama na mtoto.

Kadhalika, ulinzi na usalama wa afya ya mama na mtoto unajitokeza katika mwiko namba 32. Ijapokuwa umbo la nje la mwiko huu halimtaji mwanamke mjamzito moja kwa moja, bali mantiki inatupeleka hukohuko kwenye uzazi. Wandendeule hufuga wanyama kama vile mbuzi, kondoo na ng’ombe kwa kiwango kidogo. Katika hali ya kawaida, mnyama mwenye mimba hawezi kufikiriwa kuchinjwa; huachwa ili azae na

kuongeza idadi ya wanyama zizini. Uamuzi wa kumchinja mnyama kwa ajili ya kitoweo hufanyika kwa nadra sana. Aghalabu, mnyama huchinjwa kwa sababu maalumu kama vile kupatwa na ajali, kwa ajili ya kitoweo cha sikukuu za kidini na za kijadi au akiwa na ugonjwa unaoambukiza ili asiwaambukize wengine. Hivyo, dhana ya 'nyama ya mnyama mwenye mimba' inayotajwa katika mwiko huu inawasilisha matatizo kama vile magonjwa. Kwa mawanda mapana, mwiko huu unakataza kuliwa kwa nyama ya mnyama yeyote aliyechinjwa akiwa mgonjwa au amepata ajali. Katazo linajielekeza kwa mwanamke kutoila nyama ya namna hii kwa sababu yeye ndiye anayehusika na ubebaji wa ujauzito. Hivyo, hata kama siyo mjamzito, anapaswa kuwa makini na vyakula anavyokula ili atakapopata ujauzito isije akazaa watoto wenye matatizo yanayotokana na magonjwa hayo ya wanyama.

**33. Mwiko kwa mwanamume kukomba mwiko, ataota matiti**

Wandendeule huamini kuwa yapo mambo maalumu yanayopaswa kufanya na watoto wa kike na wa kiume. Mtoto wa kiume hakupaswa kuhusika na shughuli zozote za jikoni kama vile kupika (na shughuli zinazoambatana nayo kama vile kukomba au kuosha mwiko), kuosha vyombo au kutwanga nafaka. Aidha, mtoto wa kike hakutakiwa kushiriki katika kazi kama vile uwindaji au kulinda. Hivyo, umbo la ndani la mwiko huu linaimarisha utambuzi wa dhana za jinsi na jinsia kwa watoto.

**34. Mwiko kuonja muhindi ulioanza kuiva upande mmoja, utaugua ugonjwa wa meno**

Mwiko huu humaanisha kuwa mtoto akizoea kuonjaonja mahindi kabla hayajaiva, siku atakapotumwa kuchoma muhindi au kuchukua mahindi kwa ajili ya mgeni anaweza kufanya vivyo hivyo, hatimaye itakuwa fedheha kwa wazazi. Vilevile, akizoea kuonjaonja vitu anaweza kuwa mwizi. Hivyo, mantiki ya mwiko huu ni kusisitiza uvumilivu na heshima.

## 4.0 Hitimisho

Miiko 34 iliyojadiliwa katika makala hii inatupatia picha ya jumla kuwa miiko ni uga wenye tija katika jamii. Mjadala wa makala hii umedhihirisha kuwa miiko hujitokeza kwa namna zifuatazo: mosi, ni asasi kamili ya elimu au mafunzo juu ya mambo mbalimbali. Pili, ni kinga dhidi ya magonjwa au ajali mbalimbali. Na, tatu, ni tafsida. Aidha, mjadala umeonesha kuwapo kwa uhusiano kati ya miiko ya Wandendeule na miktadha ya maisha yao (kama vile utamaduni, jiografia [hali ya hewa na uoto], imani, matarajio, uchumi, teknolojia, pamoja na mawanda au upeo wa fikra zao kuhusu ulimwengu).

Mwisho tunatoa mapendekezo ya kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu miiko ya jamii za Watanzania kwa kujikita katika vipengele kama vile kulandana na kutofautiana kwayo, upekee, mtenguo, pamoja na unusura wa miiko ya jamii mbalimbali.

## Marejeleo


An-Nawawy, Z.Y. (2008). *Tafsiri ya Riyadhussalin – Mabustani ya Watu Wema*. Mombasa: Al-hikma For Authorship & Translation.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu.* Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Diawuo, F. & Issifu, A.K. (2005). Exploring the African traditional belief systems in natural resource conservation and management in Ghana. *Journal of Pan African Studies*. 8, 115 – 131.

Fershtman, C., Gneezy, U. na Hoffman, M. (2009). Taboos and identity: Considering the unthinkable. *American Economic Journal: Microeconomics*. 3, 139-164

Freud, S. (2004). *Totem and Taboo: Some Points of Agreement between the Mental Lives of Savages and Neurotics*. London: Taylor & Francis.

Gao, C. (2013). A Sociolinguistic study of English taboo language. *Theory and Practice in Language Studies*. 3, 2310-2314.

Hallen, B. (2002). *A Short History of African History*. Bloomington & Indianapolis: Indiana University Press.

Holden, L. (2000). Taboos: Structure and Rebellion. Mhadhara wa Wazi Uliotolewa Oktoba 2000 katika Taasisi ya Utafiti wa Tamaduni, London (Huajachapishwa).

Jacquette, D. (2006). *A Companion to Philosophical Logic*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2013). *2012 Population and Housing Census*. Dar es Salaam. National Bureau of Statistics Ministry of Finance. Inapatikana katika http://www.tzdpg.or.tz/fileadmin/documents/dpg_internal/dpg_working_g roups_clusters/cluster_2/water/WSDP/Background_information/2012_Census_General_Report.pdf

Kisanji, J.A. (2011). *Kufuwawa kwa Miiko katika Jamii za Kitanzania na Kupotoka kwa Maadili: Mfano wa Jamii ya Wabungu*. Tasnifu Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbiti, J. (1969). *Introduction to African Religion.* Portsmouth, NH: Heinemann Educational Books.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki*, *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mhaka, E. (2014). Rituals and taboos related to death as repositories of traditional African philosophical ideas: Evidence from the karanga of Zimbabwe. *Academic Research International.* 5(4), 371 – 385.

Omobola, O.C. (2013). An Overview of taboo and superstition among the Yoruba. *Mediterranean Journal of Social Sciences*. 4 (2), 221-226.

Peacock, G.G. na Wenzake (2010). *Practical Handbook of School Psychology*. New York: The Guilford Press.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ripoti ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma (1997). Ruvuma Region Socio-Economic Profile.

TUKI (2004). *Kamusi Sanifu ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Wiredu, K. (2004). *A Companion to African Philosophy*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.